

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI NA TATU

22 JUNI, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI NA TATU – TAREHE 22 JUNI, 2017

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**437. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA
(CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Sheria ya kuwalinda Wafanyakazi wa Mahotelini na Majumbani imekwama kutungwa Zanzibar na Tanzania Bara kutokana na Azimio lililofikiwa na Shirika la Kazi la Umoja wa Mataifa (ILO) kutoridhiwa na Bunge tangu Mkataba kusainiwa mwaka 2011 Mkataba ambao unataka kila Nchi Mwanachama kuwa na Sheria ya kulinda Haki za Wafanyakazi hao:-

(a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha Azimio hilo kutowasilishwa Bungeni tangu Tanzania iliposaini Azimio la ILO wakati nchi nyingine

zimeanza utekelezaji wake zikiwemo za Afrika Mashariki;

(b) Kwa kuwa Zanzibar haiwezi kutunga Sheria zake za kulinda Haki za Wafanyakazi wa Mahotelini na Majumbani mpaka Azimio hilo lipelekwe na Ofisi yako Bungeni na kuridhiwa ndiyo kila upande utunge Sheria zake kutokana na mambo ya kazi kuwa siyo ya Muungano; Je, ni lini Bunge litapokea Azimio hilo la kulinda Haki za Wafanyakazi hao;

(c) Je, Serikali inawaeleza nini Vyama vya Wafanyakazi wa Mahotelini na Majumbani ambao walianza kufanya matayarisho ya utekelezaji wa Azimio hilo lakini wamekwama kutokana na Mkataba huo kutoridhiwa na Bunge tangu kuafikiwa.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**438. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA
(SINGIDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali imekuwa na dhamira ya dhati ya kuboresha maslahi ya Watumishi hususan Walimu kwa kutoa nyaraka mbalimbali

ikiwemo Waraka wa Utumishi wa Serikali Na. 3 wa tarehe 20/10/2014 unaohusu mishahara na posho ya Madaraka kwa Viongozi wa Elimu (*Responsibility Allowance*):-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kutekeleza Waraka huo;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa posho ya kufundishia (*Teaching Allowance*) ili kuleta ufanisi wa kazi.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

439. MHESHIMIWA VEDASTO EDGAR NGOMBALE (KILWA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuitangaza Wilaya ya Kilwa kuwa ni moja ya maeneo makubwa ya Kiutalii katika Kanda ya Kusini kwa kuzingatia historia yake, maajabu mbalimbali yaliyopo, fukwe, mapango, malikale, mbuga, mabwawa na utamaduni wake.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

440. MHESHIMIWA SUZAN LIMBWEKI KIWANGA (MLIMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Katika Jimbo zima la Mlimba hakuna Mahakama hata moja, jambo linalosababisha Mahabusu kupelekwa Jimbo la Kilombero umbali wa takribani kilometa 260 kuhudhuria Mahakama:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama katika Jimbo la Mlimba ili kuwaondolea Wananchi adha ya kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma ya Mahakama.

III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na
Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017 (*The Finance Bill, 2017*).

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
22 JUNI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**